ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***SUPPLEMENT NO. 36*** ***4th September, 2020***

***SUBSIDIARY LEGISLATION***

*To The Gazette of the United Republic of Tanzania No.36. Vol.. 36 Dated 4th September, 2020*
Printed By The Government Printer, Dodoma By Order Of Government

TANGAZO LA SERIKALI Na. 739 La Tarehe 4/9/2020

SHERIA YA BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA
(SURA YA 49)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 28)*

KANUNI YA MAREKEBISHO YA BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA ZA MWAKA 2020

Jina la Kanuni Tangazo Na. 442 la mwaka 1999

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho za Baraza la Michezo la Taifa za mwaka, 2020 na zitasomwa pamoja na kanuni za Baraza la Michezo la Taifa za mwaka 1999 ambazo zitajulikana kama "Kanuni Kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 4

2. Kanuni Kuu zinarekebishwa kwenye kanuni ya 4 kwa kuongeza neno "ndogo" mara tu baada ya neno 'Kamati' lililopo katika mstari wa kwanza wa maneno ya ufunguzi na katika maneno yaliyopo kwenye maelezo ya pembeni.

Marekebisho ya kanuni ya 8

3. Kanuni Kuu zinarekebishwa kwenye kanuni ya 8 kwa -

(a) kufuta aya (b) iliyopo katika kanuni ndogo ya (1) na badala yake kuingiza aya mpya ifuatayo:

"(b) katibu wa Kamati ya Michezo za Mikoa au Kamati ya Michezo ya Wilaya ambao watapatikana kwa utaratibu ufuatao:

(i) Katibu wa Kamati ya Michezo ya Mkoa atakuwa ni Ofisa Michezo wa Mkoa au mtu yeyote anayekaimu nafasi hiyo;

(ii) Katibu wa Kamati ya Michezo ya Wilaya atakuwa ni Ofisa Michezo wa Halmashauri ya Wilaya au Halmashauri ya Mji au Halmashauri ya Manispaa au Halmashauri ya Jiji au mtu yeyote anayekaimu nafasi hizo katika maeneo hayo;

(iii) endapo katika Wilaya moja kuna Halmashauri zaidi ya moja, Mkuu wa Wilaya atakuwa na fursa ya kuteua ofisa yeyote kutoka katika halmashauri yoyote kati ya zilizopo katika wilaya husika ili kushika wadhifa wa Katibu wa Kamati ya michezo ya Wilaya";

(b) kuongeza maneno "kwa kushauriana na Baraza" mwishoni mwa kanuni ndogo ya (2);

(c) kufuta kanuni ndogo ya (3) na badala yake kuingiza Kanunia ndogo mpya kama ifutavyo:

"(3) Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya anaweza, kupokea ushauri wa Baraza kabla ya kuteua Mjumbe kujaza nafasi iliyoachwa wazi kutokana na mjumbe kujiuzulu, kuachishwa, kufukuzwa, kufa, au sababu nyingine yoyote ya msingi";

(d) kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya (3) kanuni ndogo ifuatayo:

"(4) Kazi za Mwenyekiti na Katibu wa Kamati yoyote katika Kamati za Baraza au Kamati za Michezo za Mkoa au Kamati za Michezo za Wilaya zitakuwa kama ifuatavyo:

(a) Mwenyekiti wa Kamati-

(i) kuongoza vikao na shughuli zote za Kamati katika

Baraza, Mkoa au Wilaya;

(ii) kuhakikisha vikao vya Kamati vinapangwa, kuitishwa na kufanyika kwa mujibu wa Sheria na Kanuni;

(iii) kuhakikisha maazimio ya Kamati yanatekelezwa ipasavyo;

(iv) kuidhinisha na kuwasilisha taarifa na uamuzi mbalimbali wa Kamati katika vikao vya mamlaka za juu yake;

(v) kusimamia utekelezaji wa kazi nyingine yoyote itakayoelekezwa kwake na Baraza, Kamati ya Michezo ya Mkoa au Kamati ya Michezo ya Wilaya;

(b) Katibu wa Kamati-

(i) kuitisha vikao vyote vya Kamati kwa kuandaa na kuwasilisha mialiko kwa wajumbe au vinginevyo kama itakavyoelekezwa na Mwenyekiti;

(ii) kuandaa na kuhifadhi mihutasari na kumbukumbu zingine za vikao vyote vya kamati katika Baraza, Mikoa na Wilaya vitakavyokaliwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni hizi;

(iii) kuandaa makadilio na matumizi ya rasilimali zinazohitajika katika kutekeleza shughuli za Kamati; na

(iv) kutekeleza kazi nyingine yoyote itakayoelekezwa kwake na Mwenyekiti wa

Kamati.

Marekebisho ya kanuni ya 21

4. Kanuni Kuu zinarekebishwa kwa kufuta kanuni ya 21 na badala yake kuingiza kanuni mpya kama ifutavyo:

Mapato na matumizi ya baraza.

21.-(1) Baraza la Michezo la Taifa litapata asilimia tatu (3%) ya mapato yatokanayo na mauzo ya tiketi za matukio ya michezo itakayoendeshwa na vyama mbalimbali vya Michezo, kwa ajili ya uendelezaji wa shughuli za michezo inayosimamiwa na Baraza katika ngazi za Taifa, Mkoa na Wilay, kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za michezo nchini.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1), Baraza kwa kushirikiana na Wizara au taasisi zingine zenye dhamana na usimamizi wa mapato na matumizi ya fedha za umma, linaweza kuandaa mwongozo au mpango maalum wa namna ya kukuza, kukusanya na kugawa mapato yatokanayo na shughuli za michezo kwa kuzingatia vipaumbele vya kuendeleza michezo katika ngazi za mikoa na wilaya.

(3) Pamoja na vyanzo vilivyoainishwa katika Sheria, mapato ya Baraza yatahusisha vyanzo vifuatavyo-

(a) Gawio kutoka katika mapato ya Bahati Nasibu ya Taifa na michezo mingine ya kubahatisha kama itakavyoainishwa katika Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali inayosimamia Michezo ya

*Tangazo la Serikali Na. 739 (Linaendelea.)*

kubahatisha nchini;

(b) Gawio kutoka katika mikataba inayoingiwa baina ya wadhamini na vilabu, vyama au mashirikisho kwa ajili ya udhamini na haki za kuhodhi matangazo ya televisheni katika matukio ya michezo mbalimbali kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kanuni hizi;

(c) mapato yatokanayo na miradi ya maendeleo inayobuniwa na kutekelezwa kwa ushirikiano wa Baraza, Wizara na wadau wengine kwa kuzingatia uwiano wa maslahi utakaokubalika baina ya pande husika;

(d) ruzuku au michango itakayopokelewa na Baraza kutoka kwa washirika au wadau wa maendeleo ya michezo wa ndani na nje ya nchi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali ya nchi;

(e) mapato yatokanayo na ada za usajili na ada za kila mwaka za vyama vya michezo; na

(f) vyanzo vingine vitakavyobuniwa na Baraza na kuidhinishwa na mamlaka husika kwa mujibu wa sheria."

Marekebisho ya kanuni ya 22

5. Kanuni Kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 22 kwa kufuta kanuni ndogo ya (1) na badala yake kuingiza

kanuni ndogo mpya kama ifuatavyo:

"(1) Vyanzo vya mapato vya Mfuko wa Maendeleo ya Michezo vitakuwa kama ifuatavyo-

(a) ruzuku kutoka Serikalini;

(b) ruzuku kutoka kwa washirika mbalimbali maendeleo ya michezo wa ndani na nje ya nchi;

(c) faida kutoka katika miradi ya uwekezaji itakayobuniwa na kutekelezwa na Mfuko; na

(d) ruzuku au michango itakayotolewa na Baraza kwa ajili ya maendeleo ya michezo nchini."

Marekebisho ya kanuni ya 24

6. Kanuni Kuu zinarekebishwa kwa kufuta kanuni ya 24 na badala kuingiza kanuni mpya kama ifuatavyo:

"Tozo za rufaa

24.-(1) Rufaa yoyote itakayowasilishwa katika Kamati za Michezo za Wilaya, Kamati za Michezo za Mikoa, Baraza au kwa Waziri haitatozwa gharama yoyote.

(2) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (1) mtu, klabu, chama au shirikisho lolote halitaruhusiwa kukata rufaa kwenda kwa Waziri isipokuwa kama mtu, klabu, chama au shirikisho hilo limewasilisha na kupata uamuzi wa ngazi zingine zote zilizo chini ya hatua ya Waziri kama zilivyoainishwa katika Sheria na Kanuni hizi.

(3) Utaratibu na gharama za rufaa katika vyama vya michezo mbalimbali utabainishwa na kusimamiwa kwa mujibu wa katiba za vyama husika."

Marekebisho ya kanuni ya 25

7. Kanuni Kuu zinarekebishwa kwa kufuta kanuni ya 25 na badala yake kuingiza kanuni ndogo mpya kama ifutavyo:

"Vibali vya matukio ya michezo yanayoandaliwa na wakuzaji au

25.-(1) Mkuzaji au wakala wa michezo kutoka ndani au nje ya Tanzania atapaswa kuomba na kupata

mawakala

kibali kutoka Baraza kabla ya kuandaa tukio lolote la michezo hapa nchini.

(2) Baraza kwa kushirikiana na Kamati za Michezo za Mikoa na Wilaya litaandaa mwongozo wa upatikanaji wa vibali husika kwa wakati ili kurahisisha uandaaji wa matukio ya michezo yanapofanyika katika maeneo hayo.

(3) Kibali cha kuandaa tukio lolote la michezo kinachotolewa kwa mkuzaji wa ndani au kutoka nje ya Tanzania kitalipiwa tozo kama ilivyoainishwa katika Jedwali kwenye Kanuni hizi".

Kufuta kwa kanuni ya 26

8. Kanuni Kuu zinarekebishwa kwa kufuta kanuni ya 26.

Kuongezwa kwa kanuni za 30, 31,32,33,34,35 na 36

9. Kanuni Kuu zimerekebishwa kwa kuongeza mara baada ya kanuni ya 29 kanuni mpya zifuatazo:

"Kuwasilisha mapato ya Baraza

30. (1) Chama chochote cha michezo kinachowajibika kuwasilisha sehemu yoyote ya mapato yatokanayo na tukio lolote la michezo nchini kinapaswa kuwasilisha mapato hayo kwa Baraza katika kipindi cha siku saba (7) tangu tukio hilo kufanyika.

(2) Endapo mtu, klabu, chama, shirikisho, asasi au taasisi yoyote imedhamini tukio lolote la mchezo wowote unaosimamiwa na Baraza na kuruhusu watazamaji kushuhudia mchezo huo pasipo kulipa kiingilio chochote, mtu, klabu, chama, shirikisho, asasi au taasisi hiyo itapaswa kuwasilisha katika Baraza kiasi cha fedha kilichoainishwa katika Jedwali la Kanuni hizi badala na kiasi

halisi ambacho kingetokana na asilimia ya viingilio vya watazamaji.

(3) Itakuwa ni kosa dhidi ya Kanuni hizi kwa chama chochote kukiuka kanuni ndogo ya (1), na inapothibitika chama hicho kitapaswa kulipa faini iliyoainishwa katika Jedwali la kanuni hizi.

(4) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (2) endapo chama chochote hakitawasilisha mapato yoyote ya Baraza kwa zaidi ya siku thelathini (30), Baraza linaweza kusitisha kutoa vibali vya matukio ya michezo kwa chama hicho hadi kitakapowasilisha mapato hayo na riba yake.

(5) Mtu, klabu, chama, shirikisho, asasi au taasisi yoyote ambayo haikutimiza wajibu wa kuwasilisha mapato kwa Baraza na kustahili adhabu kwa mujibu wa Kanuni hizi hataweza kuondolewa adhabu iliyoainishwa isipokuwa kama-

(a) atawasilisha maelezo ya maandishi juu ya sababu za kutotimiza wajibu huo;

(b) atawasilisha kiasi cha fedha cha msingi alichopaswa kuwasilisha kwa mujibu wa Kanuni hii;

(6) Endapo Baraza litajiridhisha juu ya ukweli wa sababu zilizotolewa na mwombaji, litamjulisha kwa maandishi msamaha wa adhabu hiyo pamoja au bila kutoa masharti yoyote.

Vibali vya kuajili wachezaji au wataalam wa kigeni

31-(1). Chama chochote kinachokusudia kuajiri na kumtumia mchezaji au mtaalamu yeyote wa michezo kutoka nje ya nchi, kitapaswa kuomba na kupata idhini ya Baraza kwa

kujaza fomu maalum na kuiwasilisha katika Baraza kabla ya kuwasilisha maombi ya vibali vya kazi na makazi vinavyotolewa katika mamlaka zingine za Serikali.

(2) Fomu ya maombi ya kibali hicho itaambatishwa na vitu vifuatavyo-

(a) maelezo na vielelezo vinavyothibitisha sifa, uwezo na vigezo vilivyotumika katika kuamua kumleta mchezaji au mtaalamu husika hapa nchini;

(b) rasimu ya mkataba unaokusudiwa kuingiwa baina ya klabu au chama na mchezaji au mtaalamu husika;

(c) stakabadhi ya malipo ya maombi ya idhini husika kama ilivyoainishwa katika Jedwali kwenye Kanuni hizi.

(3) mkataba utakaoingiwa na pande mbili chini ya kanuni hii utapaswa kurandana na rasimu iliyowasilishwa katika Baraza chini ya kanuni ndogo ya (2) (b).

(4) Maombi yanapowasilishwa, Baraza litajiridhisha juu ya sifa, uwezo, vigezo na rasimu ya mkataba uliowasilishwa na kutoa tamko katika kipindi cha siku saba (7) za kazi tangu kuwasilishwa kwa maombi husika.

(5) Idhini iliyotolewa chini ya kanuni hii haitatumika kwa klabu, chama au taasisi zaidi ya moja, endapo klabu, chama au taasisi iliyoomba

idhini husika haitakamilisha makubaliano na mchezaji au mtaalam huyo kibali husika kitakoma kutumika.

(6) Klabu, chama au taasisi nyingine ikitaka kumwajiri au kumtumia mchezaji au mtaalam aliyeshindwa kukamilisha makubaliano na klabu, chama au taasisi nyingine iliyomleta nchini kitapaswa kuomba idhini upya kumtumia mchezaji au mtaalam huyo pamoja na kulipa tozo iliyoainishwa katika Jedwali la Kanuni hizi.

(7) Itakuwa ni kosa kwa chama chochote kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria kuajiri na kuanza kumtumia mchezaji au mtaalam wa kigeni pasipo kuzingatia masharti ya kanuni hii na inapothibitika Baraza litachukua hatua zifuatazo-

(a) kutoa onyo la maandishi na kuamuru maombi husika kuwasilishwa katika Baraza;
(b) kuamuru klabu, chama au taasisi husika kulipa faini iliyosainishwa katika Jedwali la Kanuni hizi;
(c) kuamuru klabu kutoa ushauri kwa mamlaka zingine kuhusu vibali kwa mchezaji au mtaalam husika; na
(d) kusitisha vibali vya kuendesha shughuli za michezo kwa klabu, chama au taasisi husika hadi watakapotekeleza masharti husika .

(8) Masharti ya kanuni hii hayatawahusu wanamichezo na

wataalam wanaoingia nchini kwa utaratibu wa kutoa huduma za kujitolea kwa kufanya shughuli za michezo katika shule, vyuo, taasisi, asasi za umma au binafsi, vyama au mashirikisho ya michezo kupitia makubaliano mbalimbali ya ushirikiano wa kimataifa.

Mwongozo wa ajira za wachezaji na wataalam wa kigeni

32.-(1) Baraza kwa kushirikiana na mamlaka zingine za Serikali, vyama vya michezo na wadau wengine wa michezo litaandaa na kuhuisha mara kwa mara mwongozo mahususi wa kuajiri wachezaji wataalam wa michezo kutoka nje ya Tanzania kwa ajili ya kuainisha sifa, uwezo na vigezo vya wachezaji na wataalam wanaokuja kutumikia nafasi mbalimbali katika sekta ya michezo nchini.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Baraza litashirikiana na wadau kutengeneza mikataba au makubaliano elekezi ya kuajiri wachezaji, wataalam na wadhamini wa kada mbalimbali kutoka nje ya Tanzania ili wachezaji, vilabu, vyama, au mashirikisho yasiyoweza kutengeneza mikataba yao watumie mikataba hiyo elekezi.

"Udhamini kuhodhi uthamini na haki ya matangazo ya televishen

33.-(1) Chama chochote cha michezo kinachokusudia kuingia mkataba wa udhamini wa michezo au haki ya kuhodhi matangazo ya televisheni kwenye matukio ya michezo yanayoandaliwa chini yake, kinapaswa kuwasilisha katika Baraza nakala moja ya rasimu ya mkataba unaokusudiwa kuingiwa kwa ajili ya matumizi ya

Baraza.

(2) Katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria na Kanuni hizi, Baraza litakuwa na mamlaka ya kuhakiki rasimu ya mkataba wowote ulioletwa chini ya kanuni ndogo ya (1), kwa lengo la, pamoja na mambo mengine, kujiridhisha juu ya-

(a) kuzingatiwa kwa misingi ya Sheria za uwazi na ushindani wa kibiashara katika mchakato wa upatikanaji wa haki ya kuhodhi matangazo ya televisheni katika matukio ya michezo;

(b) ubora wa viwango vya huduma zitakazotolewa katika sekta ya michezo;

(c) urari wa maslahi unaonufaisha wanamichezo, vilabu, vyama au mashirikisho na unaolenga kudhibiti unyonyaji katika sekta ya michezo nchini; na

(d) uzingatiaji wa miongozo au maelekezo mbalimbali ya Serikali katika makubaliano husika.

(3) Vilabu au vyama vya michezo vitapaswa kulipa tozo ya uhakiki wa mikataba hiyo kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kanuni hizi isipokuwa tu kama mikataba hiyo inahusu Timu za Taifa.

(4) Klabu, chama au taasisi yoyote ya michezo itakayokiuka masharti yaliyotamkwa katika kanuni hii itakuwa imetenda kosa na

inapothibitika Baraza linaweza kuchukua hatua zifuatazo:

(a) kutoza faini iliyoainishwa katika Jedwali la Kanuni hizi; au

(b) kusitisha utoaji wa vibali vya shughuli za michezo kwa klabu, chama au taasisi husika kuhusiana na mkataba huo.

Uendeshaji wa timu za Taifa za michezo mbalimbali

34.-(1) Timu za Taifa za michezo mbalimbali michezo zitaundwa na vyama au mashirikisho ya michezo husika pale kunapokuwa na mahitaji ya kufanya hivyo.

(2) Baraza litashirikiana na chama au shirikisho lililounda Timu ya Taifa katika kutafuta udhamini kwa ajili ya kusaidia uendeshaji wa shughuli za timu husika inaposhiriki mashindano ya kimataifa.

(3) Vyama au mashirikisho yanayounda timu za Taifa yatakuwa na wajibu wa kuwasilisha katika Baraza mikataba ya udhamini na matangazo ya televisheni inayoingiwa kwa ajili ya timu za Taifa, ili iweze kuhakikiwa na Baraza kabla ya kuanza kutekelezwa.

(4) Itakuwa ni kosa kwa chama au shirikisho lolote kuingia na kuanza kuutekeleza mkataba wowote unaohusu udhamini au matangazo ya televisheni kuhusiana na timu yoyote ya Taifa bila mkataba huo kuhakikiwa na Baraza, na inapobainika ukiukaji huo umetendeka Baraza litachukua hatua zifuatazo-

(a) kuamuru kusitishwa kwa utekelezaji wa mkataba husika;

(b) kusitisha utoaji au utumikaji wa

vibali vya michezo husika kwa chama au shirikisho husika.

"Mchango wa michezo ya kubahatisha katika maendeleo ya michezo

36. Baraza kwa kushirikiana na mamlaka zingine pamoja na wadau wanaojishughulisha na biashara ya michezo ya kubahatisha litaandaa mpango utakaowezesha wadau wa tasnia hiyo kuchangia katika Sekta ya michezo kupitia utaratibu wa huduma kwa jamii ili kukuza maendeleo ya michezo mingine nchini."

Nyongeza ya Jedwali

10. Kanuni Kuu zinarebishwa kwa kuongeza Jendwali jipya kama ifutavyo:

*Tangazo la Serikali Na. 739 (Linaendelea.)*

JEDWALI

*(Limetungwa chni ya kanuni za 17,21,24,25,30,31,33 NA 34.)*

TOZO MBALIMBALI

| NA. | KIFUNGU | TOZO | MAELEZO YA TOZO | KIWANGO CHA TOZO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 17(1) na (2) | Kibali cha kwenda nje ya nchi au kuingia Tanzania kwa ajili ya michezo ya kimataifa. | Kibali cha kwenda kufanya tukio nje ya nchi au kuingia kufanya michezo nchini kwa vilabu vya kulipwa, | 200,000/= |
| | | | Kibali cha kwenda kufanya tukio nje ya nchi kwa mwanamichezo wa kulipwa. | 50,000/= |
| | | | Kibali cha kwenda kufanya tukio nje ya nchi au kuingia nchini kwa ajili ya kufanya michezo kwa vyama na vilabu vya ridhaa. | 20,000/= |
| | | | Vibali kwa ajili ya wanamichezo wanaoenda kwenye mashindano,matamasha au mabonanza ya taasisi za Serikali, timu za Taifa, michezo ya wenye ulemavu. | |
| 2 | 21(3)(b) | Gawio kutoka katika mikataba ya udhamini na haki za matangazo ya televishen. | Itatolewa na vilabu, vyama, mashirikisho au taasisi zinazodhaminiwa. | 1% ya thamani ya mkataba wa udhamini |
| 3 | 24(1) na (3) | Rufaa | Rufaa kwenda Kamati za michezo za Wilaya,Mkoa, Baraza na Waziri. | Hakuna tozo |
| | | | Rufaa kwenda katika vyama vya michezo. | Kiwango kitapangwa kwa mujibu wa katiba za vyama husika. |
| 4 | 25(3) | Kibali cha kuandaa matukio ya michezo kwa wakuzaji na mawakala wa ndani. | Kibali cha kuandaa mbio za marathoni na mbio nyingine za barabarani za kimataifa hapa nchini. | 1,000,000/= |
| | | | Kibali vya kuandaa mbio za marathoni na mbio nyingine za barabarani za kitaifa hapa nchini. | 500,000/= |

*Tangazo la Serikali Na. 739 (Linaendelea.)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | Kibali cha matukio mengine ya michezo ya kimataifa ambayo siyo marathoni. | 200,000/= |
| | | | Kibali cha matukio mengine ya michezo ya kitaifa ambayo siyo marathoni. | 100,000/= |
| 5 | 25(3) | Kibali cha kuandaa matukio ya michezo; kwa wakuzaji au wakala kutoka nje ya Tanzania | Maombi yatawasilishwa na mwenyeji wao. | USD 500 |
| 6 | 30(2) | Kuwasilisha mapato kwa Baraza endapo mchezo umeshuhudiwa bila kiingilio. | Itatolewa na mtu, klabu,chama au shirikisho lililodhamini watazamaji kuingia bila kiingilio katika mchezo husika. | 500,000/= |
| 7 | 30(3) | Faini ya kutowasilisha mapato ya Baraza kwa wakati | Inalipwa na chama kilichokiuka kupeleka mapato ya Baraza kwa wakati. | 1% ya fedha ambayo haijawasil ishwa |
| 8 | 31(2)(c) | Maombi ya idhini ya kuajiri mchezaji au mtaalam kutoka nje ya nchi. | Idhini itaombwa na klabu, chama au shirikisho linalomuajiri. | USD 500 |
| 9 | 31(6) | Maombi ya idhini ya kuajiri mchezaji au mtaalam kutoka nje ya Tanzania kwa klabu ambayo haikumleta nchini | Idhini itaombwa na klabu, chama au shirikisho linalomchukua baada ya kuwa ameshindwa kukubaliana au amemaliza mkataba wake na klab,chama au shirikisho la awali. | USD 1,000 |
| 10 | 31(7)(b) | Faini ya kukiuka masharti ya kuajiri mchezaji au mtaalam kutoka nje ya Tanzania. | Italipwa na klabu,chama au shirikisho lililokiuka. | USD 500. |
| 11 | 33(4) | Uhakiki wa mikataba ya udhamini na Matangazo ya Televisheni | Uhakiki utaombwa na anayedhaminiwa. | 1% ya mapato yatokanay o na mikataba husika. |
| 12 | 33(4)(a) | Faini ya kukiuka uhakiki wa mikataba ya udhamini na | Itatozwa kwa klab,chama,shirikisho au taasisi iliyodhaminiwa | 2% ya thamani |

*Tangazo la Serikali Na. 739 (Linaendelea.)*

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | matangazo ya televisheni | | ya mkataba |
| 13 | 34(3) | Uhakiki wa mikataba ya udhamini na matangazo ya timu za Taifa | Itawasilishwa na chama kinachodhaminiwa. | Hakuna tozo |

Dodoma,
25 Agosti, 2020

HARRISON G MWAKYEMBE
*Waziri wa Habari, Utumaduni, Sanaa na Michezo*